## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI AGOSTI, 2022 NA MWELEKEO KWA MWEZI SEPTEMBA, 2022.

**Dondoo za tathmini ya Agosti, 2022 na mwelekeo wa Septemba, 2022:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Agosti, 2022 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto la chini pamoja na mvua kwa mwezi Septemba, 2022 nchini.

- Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2022 maeneo mengi ya nchi yaliendelea kuwa makavu pamoja na vipindi vya baridi. Hali ya baridi zaidi ilijitokeza katika maeneo ya nyanda za juu Kusini magharibi na sehemu za miinuko za nyanda za juu Kaskazini mashariki.
- Katika mwezi Septemba, 2022 ongezeko kidogo la joto linatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, hali ya baridi inatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kusini magharibi na nyanda za juu kaskazini mashariki. Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI AGOSTI, 2022.

Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2022 hali ya baridi iliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi na nyanda za juu kaskazini mashariki yaliripoti viwango vya chini zaidi vya joto la chini.  Viwango vya joto la chini ya nyuzi joto 8°C vilipimwa katika vituo vya Igeri (kilichopo mkoani Njombe) na Uyole (kilichopo mkoani Mbeya). Halikadhalika, maeneo mengi ya nchi yaliendelea kuwa makavu. Aidha, maeneo machache ya mwambao wa pwani, ukanda wa Ziwa Viktoria na nyanda za juu kaskazini mashariki yalipata vipindi vya mvua.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

Kituo cha hali ya hewa kilichopo Mwanza kiliripoti kiwango cha juu cha mvua cha milimita 43.3 mnamo tarehe 15 Agosti, 2022. Ikifuatiwa na kituo cha Morogoro kilichoripoti milimita 28.2 mnamo tarehe 23 Agosti, 2022 Pamoja na kituo Musoma kilichoripoti milimita 25.4 mnamo tarehe 15 Agosti, 2022. Kwa upande mwingine vipindi vya upepo mkali unaofikia kasi ya kilometa 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo yakiwemo maeneo ya ukanda wa pwani na maziwa makuu.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI SEPTEMBA, 2022

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2022 hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani ikiashiria uwepo wa La Niña katika kipindi chote cha mwezi Septemba. Hali ya joto la bahari la chini kidogo ya wastani inatarajiwa katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi wakati joto la bahari la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upungufu wa upepo wenye unyevunyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani. Ingawa, hali ya joto la bahari la chini ya wastani inatarajiwa eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola lakini itakuwa na mchango hafifu wa kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani katika ncha ya Kusini mwa Afrika inatarajiwa kupunguza uwepo wa hewa yenye ubaridi kutoka Kusini.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2022

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2022 hali ya baridi ya wastani hadi joto kiasi inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, hali ya joto la chini kidogo ya kawaida inatarajiwa katika maeneo ya miinuko ya nyanda za juu Kaskazini mashariki na Kusini magharibi hususan nyakati za usiku na asubuhi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Viktoria, pwani, na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kuendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini hususan ukanda wa pwani. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 19 °C hadi 25 °C kwa maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani na kati ya 17 °C hadi 23°C katika maeneo ya nchi kavu. Aidha maeneo machache ya mwambao wa pwani yanatarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, katika maeneo ya miinuko viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa chini ya nyuzi joto 16 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.

**Kanda ya Ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 17 °C hadi 23 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita

yanatarajiwa kuwa na viwango chini ya nyuzi joto 17 ºC. Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2022.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16˚C hadi 22 ˚C katika maeneo mengi. Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 ºC hadi 20 ºC katika maeneo mengi. Hali ya ukavu na vipindi vya upepo mkali inatarajiwa kuendelea kujitokeza.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10˚C hadi 18 ˚C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ikiwemo Uyole (Mbeya) na Igeri (Njombe) yanatarajiwa kuwa na viwango vya joto la chini ya nyuzi joto 8ºC. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18ºC hadi 24ºC katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa Pwani.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14°C hadi 18°C katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya joto la chini ya nyuzi joto 14 °C. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI OKTOBA, 2022

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2022 hali ya ukavu na joto kiasi inatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.

## 2.4 USHAURI

Hali ya ukavu na upepo inaweza kuongeza upotevu wa maji kwa njia ya mvukizo na kuathiri upatikanaji wa maji kwa mazao, mifugo na matumizi mengine. Hata hivyo, tahadhari za kiafya zichukuliwe kujikinga dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na hali ya baridi na vumbi.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Septemba, 2022 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz